

# **Nguvu ya Umma: Utangulizi**

Civil Resistance: A First Look

Originally published by ICNC, 2011

**Translation: JPD Systems, April 2019**



# Nguvu ya Umma: Utangulizi

**Ni nini?** Nguvu ya umma ni namna ya wananchi wa kawaida kupigania haki zao, uhuru, na usawa bila kutumia - njia za mizozo. Wananchi wanaotumia nguvu ya umma hutumia mbinu mbalimbali, kama vile migomo, kususa, maandamano makubwa na hatua nyingine, ili kuleta mabadiliko makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Duniani kote, nguvu ya umma imekuwa ikiitwa kwa majina mbalimbali kama —mapambano ya kudai haki kwa njia ya amani, kujichukulia sheria mkononi, nguvu ya raia, , na mkakati wa kudai haki bila kuvunja sheria, na wananchi kuungana kwa sauti moja —lakini kwa vyovyote vile utakavyo i ita, kikubwa ni kujua kuwa mienendo ya msingi ya nguvu ya umma inabaki ile ile tu.

Maandamano yenye kutumia nguvu ya umma yanaogopesha kwa sababu huwakusanya watu wengi pamoja kupinga uonevu na mateso yenye kuletwa na viongozi kwa kuleta dira mpya ya jamii yenye uhuru na haki zaidi napenginekutoendelea kuwaunga mkono wale walioidhinisha mfumo wa zamani. Watu wengi wanapoamua kutowaunga mkono watawala wabaya, ufanyaji kazi wa mfumo huo huwa ngumu sana. Pale watu wanapoamua kutotii, mfumo unaweza kuwa siyo endelevu, na mwishowe lazima ubadilike au

uanguke.. Hata pale wale wanaopinga nguvu ya umma kwasababu wana kuwa na silaha na fedha za kutosha, mara

*“Jambo la msingi katika mapambano ni kuonekana na watuunaopambana nao.. Kupambana ukiwa umejificha kwenye kona ambapo huonekani ni juhudi zisizozaa matunda. Lazima — kama unapambana —uoneshe kadri uwezavyo kinachosababisha upambane.”*

—MKHUSELI JACK, KIONGOZI KWENYE KAMPENI ZA KUGOMEA

nyingi wamekuwa wakishindwa kukabiliana na maandamano ya kutotii sheria zenye mateso yaliyoandaliwa na wananchi waliosimama pamoja.kudai haki kwa amani.

Kwa sababu hiyo, harakati nyingi za matumizi ya nguvu ya umma pamoja na kampeni nyingi yamefanikiwa dhidi ya wapinzani mbalimbali.. Kwa kila miaka kumi ya ya karne iliyopita, katika mabara sita ya dunia, maandamano yenye kutumia nguvu yaliyojuliakana sana kwa kuzivunja tawala zenye nguvu, kwa kupinga uvamizi wamajeshi, na kuleta haki kubwa na uhuru kwa jamii zao kwa njia ya amani Kwa mfano, matumizi ya nguvu ya umma yalisaidia sana katika kutokomeza ubaguzi wa rangi Afrika Kusini;ilitumika kutetea haki za wanawake, haki zaraia, na haki za wafanyakazi nchini Marekani; yalisababisha kupungua udikteta Ufilipino, Chile, Indonesia, Serbia na maeneo mengine; yalitumika katika kuzuia mataifa ya

nje kuvamia Denmark na Timor ya Mashariki; ilikuwa msaada kwa India katika kudai uhuru kutoka kutoka kwa Mwingereza; imesaidia kutupilia mbali chaguzi zisizo huru na haki Ulaya Mashariki , ilitokomeza uvamizi wa Syria nchini Lebanon, na imetumika kwenye nchi nyingi tu kuleta haki za binadamu, sheria ya kweli, na utawala wa kidemokrasia.

## Dhana Kuu

**Nguvu ya Umma dhidi ya Kudai Haki kwa Njia ya Amani** Nguvu ya umma ni aina ya ubishi wa kisiasa.

Kudai haki kwa njia ya amani ni mfumo wa kanuni zinazozuia matumizi ya nguvu yoyote.

Wahusika katika maandamano ya kudai haki yaliyofanikiwa kwa kutumia amani , kwa mfano Harakati za kudai Uhuru nchini India na watumia nguvu ya umma nchini Marekani, wamesistiza kudai haki kwa njia yaamani . Hata hivyo, si asili kwamba katika kutumia nguvu

ya umma siku zote waandamanaji watahakikisha hawavunji amani. Kwakweli, kihistoria, inawezekana kabisa kwamba raia wengi waliopinga kuonewa hawakupendelea kudai haki kwa njia ya amani. Badala yake, walipenda kutumia mabavu kama njia pekee na yenye ufanisi kwao katika kufanikisha mapambano yao.



## Mtazamo wa Dola Moja dhidi ya Dola la Wananchi

Katika jamii nyingi, mtazamo unaotamba ni ule wa kutawaliwa na dola moja (MCHORO WA 1), yaani wananchi wa kawaida wanategemea matwakwa, maamuzi, na msaada wa serikali yao

na taasisi nyingine. Nguvu inaonekana ikitumiwa na wachache ambao wanakuwa kileleni katika kutoa matamko, wenye kujilimbikizia mali na kutumia nguvu. Mtazamo wa dola moja huonekana kujimulika lenyewe, la kudumu na si rahisi kubadilika. Hata hivyo, nguvu ya umma imejikita katika mtazamo mwingine, unaoelezwa kwa kupitia mtazamo wa dola la wananchi (**MCHORO WA 2**), ambalo linaziangalia serikali na mifumo mingine ya kiutawala kama tegemezi sana kwa matakwa au makubaliano ya wananchi. Kwenye mtazamo wa dola la wananchi, nguvu inaonekana inategemea maamuzi na uwepo wa makundi mengi ya jamii.

Una ugiligili, siku zote kupata kwake nguvu hutegemea vyanzo vyake kwa kutumia ushirikiano wa taasisi nyingi na watu. Hivyo basi, matumizi ya nguvu ya umma hujtengenezea mikakati yake kwa kujikita kimawazo kwamba wananchi ambao huunda mseto mkubwa wa wananchi wa kawaida na kusababisha shughuli za serikali kusimama wanaweza wakasawazisha mambo au wakabadilisha mtazamo.

**Migomo Baridi na Vitendo vya Uvunjifu wa Amani** Watu wanaopinga uonevu wamekuwa wakitumia mamia ya mbinu mbalimbali kwa muda mrefu. Mbinu hizi zinaweza kuwekwa katika makundi mawili. Migomo baridi ni mbinu ambazo watu husisa kufanya jambo fulani ambalo walitarajiwa kufanya au wanatakiwa kufanya. Mifano ya vitendo hivyo ni pamoja na migomo, kukataa kulipa kodi, na kususia bidhaa. Vitendo vya uvunjifu wa amani ni mbinu ambazo watu huhusishwa kufanya vitu ambavyo siyo kawaida yao kufanya au ambavyo hawaruhusiwi kufanya. Mifano ya vitendo hivyo ni pamoja na migomo, maandamano makubwa, kujibweteka, na aina nyingine ya uvunjifu wa sheria. Namna ya ufyatiliaji wa mbinu hizi huongeza gharama kwa wenye kupinga matumizi ya nguvu ya umma katika kukabiliana na hali hiyo. Wananchi wa kawaida pia huhamasishwa kushiriki mgomo, kwakuwa mbinu zinaweza kuwa mbali mbali—zenye hatari kubwa na ndogo, zenye kuhusisha umma au taasisi binafsi, zenye kuwaweka wengi pamoja au kwa makundi

makundi—ambazo huwezesha watu kutoka makundi mengi ya jamii kushiriki..

### **Umoja, Kuweka mipango na Kuwa na Ukimya katika Kudai haki**

Mambo makuu ya kuleta mafanikio katika kutumia nguvu ya umma ni umoja, kuweka mipango na na kuwa na ukimya katika kudai haki . Umoja unatengenezwa kwa kuwaleta watu pamoja kutoka sehemumbali mbali za jamii, ambao mwanzoni wanaweza kuwa na manung'uniko tofauti, lakini wana kitu kimoja chenye malengo ya ushindi. Kuweka mipango ni namna ya kufuatilia kampeni na mbinu kwa kuzingatia uchambuzi makini wa masharti na fursa katika kufanya hivyo. Na pia inahusisha kubashiri uwezekano wa vikwazo na kuweka mipango ya dharura kwa ajili ya hivyo vikwazo.

Maandamano ya amani huhusisha maamuzi ya kimkakati katika kutumia njia za amani tu, kwa sababu ghasia hupunguza ushiriki wa raia, hufifisha uhalali wa matumizi ya nguvu ya umma , hupunguza kuungwa mkono na jumuiya za kimataifa, na hupunguza uwezekano wa kubadili uungaji wa mkono.

### **Maswali Kumi**

#### **1 Je, watawala wenye nguvu wanashindwaje na wananchi wa kawaida wanaotumia nguvu ya umma?**

Hakuna mtawala mwenye nguvu sana kiasili . Watawala wana nguvu tu wakati wanaposaidiwa na maelfu au mamilioni ya wananchi kwenye jamii yao au kwa kutumia mlango wa nyuma.Ili mtawala aweze kudhibiti, lazima kazi ifanywe vema na polisi, jeshi, mahakama, na urasimu. Watu kwenye jamii nzima wanapaswa kwenda kufanya kazi kila siku, walipe kodi serikalini na kodi za pango, na wanunue vitu kwenye masoko ambayo yanasaidia biashara zinayomilikiwa na serikali. au ambazo leseni zake zinatolewa na hiyo serikaliWatu wanaofanya kazi kwenye bandarini na kwenye usafirishaji, pamoja na kwenye mawasiliano

na kwenye huduma, lazima waendeleo kusafirisha bidhaa na kufanya huduma. Hii ni mifano michache tu kati ya makundi mengi ambayo hutoa msaada ili mfumo ufanye kazi vema.

Kwa kulielewa hili, waandaaji wa nguvu ya umma huweka mikakati ya kuivuruga misaada hiyo na kusababisha hali kwenda mrama. Kuwaleta watu wengi kuwa na sauti moja kwenye kupinga na kugoma hupunguza uhalali wa watawala, hasa ikiwa ukandamizaji hutumiwa dhidi ya watu wanaodai haki zao. Kuharibu msimamo wa serikali, matumizi ya nguvu la umma yanaweza kuimarisha gharama za kuurejesha mfumo—hadi kufikia hatua ya askari wake kuwa na wasiwasi wa yatakayotokea kesho yake. Mara baada ya uaminifu wao kupotea, inakuwa ngumu zaidi kutumia njia yoyote ya ukandamizaji.

## **2 Je, nguvu ya umma huanzaje?**

Kampeni nyingi kuhusu matumizi ya nguvu ya ia umma ambazo zinafanikiwa huanza kwa kuwajengea uwezo wananchi wa kawaida kuchukua hatua. Mbinu za wananchi wa eneo fulani, zenye madhara kidogo kutumika kuwakusanya watu na kujenga umoja zinaweza kuwa muhimu sana. Kwa mfano, kabla ya Gandhi kuitisha kampeni zake za kwanza za kutumia nguvu ya umma nchini India, alitumia miezi na miaka akiwatembelea wananchi wa kawaida na kuongea nao, huku akipata manung’ uniko yao, matumaini na hofu zao. Alitengeneza mazingira ya kuwafanya wamwamini na kutoa ushirikiano wao. Pia aliwatia moyo watu wafanye “kazi za maendeleo”— huduma kwa jamii ambayo ilisababisha kujitegemea baina ya watu waliokuwa wamepoteza matumaini na serikali lakini waliokuwa wanajihisi hawakuwa na uwezo wa kuchukua hatua ya kufanya kitu.

Mara kampeni zimefanikisha kwa kiasi cha kujenga uwezo wa kushiriki kwenye nguvu ya umma, mara nyingi huanza na mambo ya kawaida ambayo yanahusu umma zaidi. Kwa mfano, waandaaji wa Solidarity (yaani mshikamano) nchini Poland walianza na



mgomo wa wafanyakazi kwenye kampuni ya kutengeneza meli. Baada ya kufanikisha, ushindi huo ulileta mafanikio makubwa sana ya kisaikolojia kwa Wapolandi nchi nzima na na matumizi ya nguvu ya umma yalipamba moto.

Vivyo hivyo, kudai haki za raia nchini Marekani kulipata nguvu zaidi kufuatia mafanikio ya migomo baridi na masusio ambayo yalimaliza ubaguzi wa rangi kwenye maduka na mabasi kwenye miji kadhaa kusini mwa Marekani. Kwa kupitia mafanikio haya, kudai huku kwa haki kulionesha uwezo la nguvu ya umma na taifa zima liliweka umakini kwenye ufuatiliaji.

### **3 Naweza je kuanzisha na kuandaa maandamano?**

Wanao panga matumizi ya nguvu ya umma wanapaswa kutambua malengo yao ni nini hasa, faida ni zipi, hasara na uwezo wao na uwezo wa wanaopambana nao, na msaada gani watu wengine na wapembeni wanaweza kuwapa. Maramikakati ikishaonesha wazi malengo yake ya muda mfupi, ya muda wa kati na ya muda mrefu, na uchambuzi yakinifu na wenye utaratibu maalum umeshafanyika juu ya hali halisi, hapo litakuwa katika nafasi bora ya kuchagua mbinu gani itumike. Kwa wakati huu, kama watumia nguvu ya umma imeamua kutumia maandamano yenye mgomo ndani yake kama mbinu kuu na wanataka kuona namna ya kufanikiwa, kuna rasilimali nyingi zenye kusaidia mbinu za kiufundi na za katika kutekeleza hilo.

### **4 Kama si maandamano, nini kifanyike basi?**



Watu wengi hudhani maandamano ndo kitu cha msingi kwenye matumizi ya nguvu yaumma . Hata hivyo, maandamano ni moja tu ya aina mbalimbali za mbinu ambazo watumiaji wa nguvu ya umma wanaweza kutumia katika mapambano yao. Kuna zaidi ya mbinu mia mbili za mapambano kwa njia ya amani ambazo zinaweza kutumika.

Aina za kususa (bidhaa, kisiasa au kijamii); migomo; kupunguza utendaji kazi; kukataa kulipa kodi na kodi za pango, kutoa ushuru; kuweka sains za pamoja kumshinikiza kiongozi; kutotii sheria bila shuruti; migomo baridi; kufunga njia; na ongezeko la taasisi

mbadala ni mifano michache tu ya mbinu za kutumia nguvu ya umma.

Uchaguzi na namna ya kufuatilia mbinu hutegemea tathmini ya hali halisi ya matendo, pia uwezo na malengo yake. Kama matumizi ya nguvu ya ummasi kubwa sana, matumizi ya mbinu za kudai haki kwa kutawanyika na yenye hatari kiasi kidogo yanaweza kutumika, kama vile migomo au kuweka maandishi ya mafumbo ili kukuza maandamano, kufikisha ujumbe, na/au kumkwamisha mpinzani. Baadaye, nguvu inapokua kubwa zaidi, aina nyingi za mbinu ya kukusanyika pamoja zinaweza kutumika, kama vile mikutano ya upinzani, kuingia barabarani, mandamano yenye migomo ndani yake, au wengi kutotii sheria bila shuruti. Ni muhimu kukumbuka kwamba kwakuwa migomo ndo hatua kuu zinazojulikana kwa watu kwamba ndo nguvu ya umma yenyewe, si kwamba basi ndo mbinu pekee au nzuri zaidi za kufanikisha mambo. Kuna mbinu nyingine nyingi ambazo zinaweza kutoa matokeo bora zaidi kwa kutumia gharama ndogo tu. Ubunifu na tafakuri tunduizi ni muhimu sana katika kuamua mbinu gani za kutumia.

## **5 Je, kama kwenye matumizi ya nguvu ya umma hakuna kiongozi mwenye karama?**

Matumizi ya nguvu ya umma mengi ya kihistoria yalifanikiwa bila kuwa na viongozi wenye karama. Kupinga ubaguzi wa rangi Afrika Kusini kulifanikiwa sana ingawa kiongozi wake alikuwa gerezani, na hivyo hakushiriki kwenyemaandamano hayo. Kikubwa zaidi ya ndumba binafsi au uwezo wa kuongea wa viongozi kwenye maandamano yanayohusisha wananchi ni elimu ya namna kuwakilisha na kuwasikiliza walio wengi kwenye maandamano, kupima kwa umakini gharama na shida zinazoweza kujitokeza wakati wa kukabiliana, na kushirikiana na viongozi wengine katika kufanya maamuzi.

Kwa kuongezea, kuwategemea sana viongozi wenye karama huleta shidaza kipekee. Mara nyingine viongozi kama hao huteuliwa na watawala kwa kuwahonga madaraka ya uongozi, u

wanaweza kukamatwa. Maandamano yenye uvumilivu na yenye uwakilishi huandaliwa ili kwamba hata kama viongozi wamekamatwa, bado matumizi ya nguvu ya umma yanaweza kuendeshwa na viongozi wengine wapya.

## **6 Je, kama siamini nguvu ya umma itafanikiwa nchini mwangu?**

Si kwamba nguvu ya umma itafanikiwa siku zote. Hata hivyo, imefanikiwa katika nchi nyingi duniani ambapo “wataalam” na wengine walifikiri yasingefanikiwa. Generali Augusto Pinochet wa Chile alikuwa anachukuliwa mmoja wa madikteta hatari sana duniani, na watu wengi hawakuamini kwamba nguvu ya umma ingeweza kuwa muhimu katika kumwondoa madarakani, lakini ndivyo ilivyokuwa. Wachache pia walitegemea dikteta Slobodan Milosevic wa Serbia, aliyepewa jina la utani “Mchinjaji wa Balkani”, angeondoshwa kwa nguvu ya umma. Cha kushangaza, Milosevic alivyowaamuru majeshi na polisi wake mwenyewe wawatishe mamia kwa maelfu ya waandamanaji waliokuwa wanataka aondolwe madarakani mwaka 2000, lakini vyombo vyake vya usalama vilikataa kutii mamlaka mbele ya wananchi wenzao waliokuwa wamejipanga kwa wingi. Kwahiyo Milosevic hakuwa na namna nyingine zaidi ya kuacha tu uongozi.

Kama bado huna uhakika kwamba nguvu ya umma itafanikiwa kwa upande wako, basi tumia mbinu zinazoweza, ili mradi tu ni za uhakika: kubadili mfumo wa siasa za ndani; kuwemo kwenye chaguzi; kuupigia kelele mfumo wa sheria; kuingia kwenye majadiliano na midahalo na washindani; kuomba msaada kutoka kwa jumuiya ya kimataifa; na kujaribu kutumia maandamano yenye kutumiasilaha ni njia ambazo zimetumiwa sehemu nyingi duniani. Wakati hatuna uhakika kama nguvu ya umma itafanikiwa, pia hatuna uhakika kama mbinu fulani kati ya hizo itafanikiwa.

Kwa hiyo, maamuzi ya wapambanaji ni kuchagua mbinu ambayo inaonekana kufanikisha wafuasi mbali mbali, kuhoji uhalali wa mtawala, kuepuka au kupunguza kamatakamata, na kuwagawa wale wanaoutetea mfumo uliopo. Kwa kipindi kirefu

kumekuwepo kwa makundi mengi ambayo yameangalia njia hizi na kuamua kutumia nguvu ya umma, ingawa mara kadhaa wameitumia pamoja na njia nyingine za kiasili za kufanya mabadiliko kisiasa, kwa mfano chaguzi, kuipigia kelele sheria, majadiliano, na kubadili mfumo wakiwa ndani.

## **7 Je, kama mpinzani atatumia mabavu?**

Kuna umuhimu wa kutambua kwamba kuna kipindi mpinzani wako atatumia mabavu. Historia inatukumbusha kwamba hiyo ndo imekuwa jadi. Hata hivyo, mpinzani kutumia mabavuhaimaanishi matumizi ya nguvu ya umma yameshindikana. MNguvu ya umma hukabiliana na vitisho vya mabavu kwa njia nyingi ambazo hupunguza makali yake na/au kumgeuzia kibao mkandamizaji.

Ya kwanzak, ili kuepuka au kuzimisha matumizi ya mabavu, matendo ya kutumia nguvu ya umma yanaweza yakaanza kutumia mbinu ambazo ngumu kuzuia kwa kutumia mabavu. Kwa mfano, migomo ya kununua bidhaa ambapo wananchi wanaweza kuamua kutonunua aina fulani za bidhaa ni ngumu kuizimisha, kwa sababu imegataliwa na ni ngumu au haiwezekani kwa dola kugundua nani anashiriki kwenye mgomo na nani hashiriki. Maandamano yenye mgomo ndani yakeau mbinu nyingine zenye kuwakusanya pamoja watu wengi yakizuiliwa, mgomo usio wa kisiasa au mbinu zilizogataliwa na zisizoonekana wazi kama vile kugoma kulipa ada au kodi au hata mgomo wan chi nzima zinaweza kuwa njia sahihi za matumizi ya nguvu ya umma.

Ya pili, nguvu ya umma inaweza kutumia mbinu za hali ya juu ili matendo ya mabavu ya mpinzani ya mgeukie mwenyewe..., Kuitangazia dunia juu ya ukandamizaji wa haki, kwa kuonesha ugandamizaji huo kwa njia ya picha na habari za ndani ya nchi, kunaweza kuigharimu zaidi nchi—kwa maana ya heshima kimataifa na uwekezaji— kuliko matumizi ya nguvu ya umma. Si kila ukandamizaji humrudi mpinzani ama mhusika, bali matumizi ya nguvu ya umma yanapopamba moto, huchelewesha, au huonesha vitendo vya uasi; matokeo yake yanaweza kuwa ni

*“Ndiyo maana kibao kiligeuka kwa uminyaji huu wa haki.  
Kwa sababu ulikuwa kama sheria ya tatu ya mwendo ya Newton.  
Unapokuza kiwango cha uminyaji haki, kukabiliaana huongezeka pia”*

—IVANMAROVIC

kupoteza sana uungwaji mkono wa mpinzani na wananchi pamoja na jumuiya ya kimataifa.

Ya tatu, kuna umma, kwa mfano Wafilipino mwaka 1986, Chile mwaka 1988, Serbia mwaka 2000, naUkraine mwaka 2004, ambapo vikosi vya usalama viliwasaidia wanao waandamanaji, ambao walipunguza au kutokomeza kabisa ukandamizaji wa haki. Ukengeukaji wa vikosi vya usalama haukuwa wa bahati mbaya, bali ilikuwa ni matokeo ya juhudi za muda mrefu yenye kupingauonevu ambayo yalisababisha vikosi vya usalamakutounga mkono serkali.

## **8 Je, kama mpinzani wanguasiposhawishika?**

Si lazima kuwashawishi wale viongozi wa wanaohisika na ukandamizaji wa haki, ili kushinda. Hata hivyo, pengine ni muhimu kuwashawishi baadhi ya wale wanao shiriki na kumuunga mko mpinzani wako.

Kumbuka, nguvu ya umma ina kishindo kwa sababu hubadili imani na tabia ya maelfu au makumi ya maelfu ya watu ambao matendo yao huunga mkono ukandamizaji moja kwa moja au kwa namna nyingine. Vyanzo vya nguvu vya mpinzani wako vinapopungua nguvu, hapo iwe ameshawishiwa au la kuna mabadiliko kiasi. Nguvu yake inakuwa imepungua kiasi cha kugundua kwamba hawezi kuzuia matokeo, na hapo sasa analazimika kujadili mambo ya mpito upya.

Kwa mfano, mwaka 1985 mgomo wa kususia bidhaa za wazungu wakati wa kupinga ubaguzi wa rangi kwenye mji wa Port Elizabeth, Afrika Kusini ulisababisha hasara kiasi kwamba serikali ikaanza kupigiwa kelele kubadili sera zake. Wafanya biashara

hawa huenda hawakushawishiwa kukubaliana na malengo ya matendo hayo, bali waligundua inaingia akilini mwao bora kukubaliana na matakwa ya matumizi ya nguvu ya umma kuliko kuendelea kukubaliana na ukandamizaji unaofanywa na serikali.

*“Kwakweli kulikuwepo na watu lukuki ambao walileta mabadiliko Afrika Kusini*

*... ambayo yaliinyima usingizi nchi...hatimaye ikabadilika... [kuleta] utulivu, kukwama ambapo nchi haikuwa na usemi wowote tena.” —DK. JANET CHERRY*

## **9 Hii itachukua muda mrefu sana. Nini ifanyike, kama hatuwezi kusubiri?**

Nguvu ya umma huwa haichukui muda mrefu kuleta matokeo mazuri. Pamoja na kwamba Vuguvugu la “Solidarity” lilichukua kama miaka kumi ndipo likapata nguvu tangu kuanzishwa kwake, ilichukua miaka michache tu kwa Wafilipino kumtoa madarakani dikteta wao, Ferdinand Marcos. Kinachosababisha mafanikio kwenyematumizi ya nguvu ya umma si muda, bali matendo yenye watu walio na umoja na mikakati kwenye kuchukua hatua.

## **10 Je, tunawezaje kushinda?**

Mnaweza kushinda kirahisi kama matendo yenu au kampeni zenu zinatengeneza umoja thabiti, mnapangilia mambo vizuri, na mnakuwa na maandamano ya amani katika kudai haki .

Umoja ni muhimu sana kwa sababu matumizi ya nguvu ya ummayana nguvu pale yanapowakilisha matakwa na maamuzi ya wengi. Ni muhimu kukumbuka kwamba kujihusisha na matendo haya ni kwa utashi pekee wa mtu, na siyo kwa ku lazimishwa. Watu hujiunga na kuamua litakalokuwa na liwe kwa sababu wanaliamini tendo lao. Hata hivyo, umoja usipokuwepo, kama sababu haieleweki au bado inatia mashaka, wengi hawataunga

mkono. Kwa ujumla, nguvu za umma zilizofanikiwa kwa zimewaleta pamoja wanaume na wanawake; watoto, vijana, na wazee; watu kutoka dini na kabila ama maadhili tofauti; wanafunzi, wafanyakazi, wasomi, wafanyabiashara na wengineo.

Kuweka mipango ni muhimu sana kwa sababu nguvu ya umma ni ushindani kati ya kinara kama vile kampeni, matemdo, au kundi la kijamii, na wapinzani wake. Katika ushindani huo, mipangilio na mikakati vinahitajika sanakatika kutengeneza nguvu na kuisukuma kwa wananchi watacao husika na matendo hiyo.. Katika kutumia nguvu ya umma, viongozi huwa na maamuzi mengi yanayotegemea mikakati na mbinu, ikiwa ni pamoja na namna ya kutengeneza rasilimali, namna ya kuzitumia kwa ufasaha hizo rasilimali, namna ya kutumia udhaifu wa wapinzani wao, na namna ya kujihami dhidi ya adui kulipiza kisasi. Ni mara chache maamuzi sahihi hutokea hapo hapo. Ili kuweka mipango sawa, inatakiwa elimu ya aina mbili. Kwanza, wapanga mikakati wanahitaji kuwa na ujuzi wa kina hali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii wanayokumbana nayo, na wanahitaji kujua matakwa na matumaini waliyo nayo makundi mbali mbali katika jamii. Pili, wapanga mikakati katika matumizi ya nguvu ya umma wanatakiwa kujua namna nguvu hiyo inavyofanya kazi, na hii mtu anaweza kujifunza kupitia uzoefu binafsi, kutoka kwenye rasilimali kama vitabu, filamu na to mtandao wa "internet", na wa kuwasiliana na wengine wenye uzoefu kwenye masuala ya nguvu ya umma na kuwaleta watu pamoja kisiasa.

Mwenendo bora kati ya matumizi ya nguvu ya umma. Mwenendo bora na wa amani ni muhimu sana kwa kuwa matumizi ya mabavu katika vuguvugu hudhoofisha mapambano; mara nyingi huonekana kuhalalisha kufifisha nguvu ya wapinzani. Zaidi ya hilo, wakati vuguvugu linaanza kutumia mabavu, hii hupoteza washiriki katika jamii ambao kwa kawaida wasingependa kupata hasara kupitia matumizi ya nguvu. Mwisho, vuguvugu likitumia mabavu kukabiliana na polisi na jeshi, inakuwa vigumu kuwatenganisha watetezi wa wanyonge wa mfumo, na hivyo huruma yoyote ya chinichini juu ya vuguvugu baina ya hao watetezi ni rahisi kupotea. Hii ni kinyume cha ile kuruhusu kwamba nguvu ya umma



inaweza kutumika, ambapo sababu ya vuguvugu — jamii huru na nzuri zaidi inayomnufaisha kila mtu— na hatua za matumizi ya nguvu ya umma, kuwapa motisha wananchi wa kawaida kutoka makundi yote, kuwa kivutio kwa watetezi wengi wenye mamlaka kama ilivyo kwa wanaotaka kuuzimisha mfumo.

Громадянська  
Kig  
damheid: een eerste blik  
民間性: 先看看  
المقاومة للمد  
burgerlijke gra  
civilisatie: un  
civile: un primo sguardo  
awam pertahanan  
гляд kiralia  
ньське